

JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2322703
Nukushi: +255 26 2322704
Barua Pepe: km@uchukuzi.go.tz
Tovuti: <https://www.uchukuzi.go.tz>



Mji wa Serikali – Mtumba,
1 Mtaa wa Ujenzi,
S. L. P. 638,
40470 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

MAADHIMISHO YA WIKI YA USALAMA WA RELI
TAREHE 09 - 13 OKTOBA, 2023

Mpanda, Katavi

Tarehe 08 Oktoba, 2023

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Uchukuzi na Taasisi zinazosimamia masuala ya usalama wa reli inatarajia kuadhimisha Wiki ya Usalama wa Reli Kitaifa katika Viwanja vya Taasisi ya Teknolojia ya Reli Tanzania (TIRTEC), mkoani Tabora kuanzia tarehe 09 hadi 13 Oktoba, 2023.

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatambua umuhimu wa usafiri wa Reli na imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya usanifu, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Reli na uendeshaji wa shughuli za Reli nchini.

Serikali imesimamia suala la usalama wa reli katika hatua za ujenzi pamoja na uendeshaji na kuimarisha ulinzi wa miundombinu ya reli kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya uchukuzi na Wananchi ili kudhibiti ajali zinazoweza kuzuilika.

Tanzania ikiwa nchi mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kupitia Shirikisho la Reli za Kusini mwa Afrika (SARA) imekuwa ikizingatia na kufuata Sheria na Kanuni za usalama wa uendeshaji wa shughuli za Reli pamoja na maazimio na miongozo ya SARA. Kuadhimisha Wiki ya Usalama wa Reli mwezi Oktoba kila mwaka, kaulimbiu ya maadhimisho kwa mwaka 2023 ni “**USALAMA UNAANZA NA WEWE; CHUKUA TAHADHARI**”.

Wadau wa usafiri wa Reli na wananchi hususani wa Mkoa wa Tabora na mikoa ya jirani wanaombwa kujitokeza kwa wingi katika maadhimisho haya ili kujifunza na kupata uelewa wa masuala mbalimbali ya usalama wa Reli. Watumiaji wa huduma za Reli na wananchi wanahimizwa na kukumbushwa kuwa makini, waangalifu na kuchukua tahadhari za kiusalama wanapotumia huduma za usafiri kwa njia ya Reli wakiwa kwenye vituo vya treni, ndani ya mabehewa na hata wanapopita karibu na maeneo ya Reli kwa kuwa usalama unaanza na mtu binafsi.

Tuunge mkono juhudi za dhati za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika uwekezaji unaoendelea ili kuboresha miundombinu ya Reli na kukuza uchumi wa Tanzania.



Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb.)
WAZIRI WA UCHUKUZI